

## Maswali

1. Mfalme wa Uajemi alikuwa nani?
2. Malkia alikua nani?
3. Mfalme Ahasuero aliamrisha nini kwa siku ya saba ya karamu yake?
4. Malkia Vashti alifanya nini?
5. Mfalme aliadhibu Vashti namna gani?
6. Wajumbe walileta nani kuishi kwa nyumba ya kifalme Shushani?
7. Mordekai alipeleka nani kuishi kwa nyumba ya kifalme.
8. Mordekai aliambia Esta asiambie mtu yeyote nini?
9. Mfalme alichagua nani kuwa Malkia mpya?
10. Mordekai alikundua nini?

## Majibu

1. Ahasuero alikuwa Mfalme wa Uajemi.
2. Vashti alikuwa Malkia.
3. Kwamba Vashti avae taji ya kifalme na aje kwa karamu yake.
4. Vashti alikataa kuenda.
5. Vashti hakukubaliwa kuwa Malkia tena.
6. Wajumbe walileta wanawake warembo wote kwa nyumba ya kifalme.
7. Mordekai alipeleka binamuye mdogo, Esta kuishi kwa nyumba ya kifalme.
8. Esta asiambie mtu kwamba yeye ni Myahudi.
9. Mfalme Ahasuero alichagua Esta kuwa Malkia mpya.
10. Mordekai alikundua kwamba kulikuwa na watumishi wawili waliopanga kuu mfalme.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2



## 86 Esta anakuwa Malkia

### Kwa Biblia

Esta mlango wa 1 na 2

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu analinda watu wake. Anafanya mambo yafanyike ili aokoe watu wake, Wayahudi

### Somo

Somo lililopita tulisoma vile Wayahudi wengi walienda kuishi kwa nchi ya Israeli. Lakini kuna Wayahudi wengine waliofuhia kuishi kwa nchi waliyopelekwa kama watumwa. Hawakutaka kurudi kwa nchi ya Israeli. Esta alikuwa mmoja wa Wayahudi waliobaki. Esta aliishi kwa mji wa Shushani. Shushani ulikuwa mji mkuu wa Uajemi.

Ahasuero alikuwa Mfalme wa Uajemi. Ahasuero alikuwa mtawala wa nguvu. Alitawala saidi ya maeneo 127. Mfalme Ahasuero aliishi kwa nyumba ya kifalme ya Shushani. Kila mtu alitii Mfalme Ahasuero iwezekanavyo.

Mfalme Ahasuero alikuwa na sherehe kubwa kwake. Alialika wakuu wa utawala wake. Nyumba ya kifalme ilikuwa nzuri sana. Nguzo za marmar (mawe mazuri yanayong'aa) yalipambwa kwa rangi ya majano, samawati na nyeupe. Sakafu ilitengenezwa kwa marmar na mawe mengine ya dhamana. Wakuu na watawala walilala kwa matandiko ya dhahabu na fedha. Kila mtu alikunyua kwa vikombe vya dhahabu. Hiyo karamu ilikuwako kwa siku saba.

Vashti alikuwa Malkia. Vashti naye alifanyia wanawake wa nyumba ya kifalme karamu. Wakati huo kulikuwa na desturi kwamba wanawake walitengwa kutoka kwa wanaume. Ilikuwa mwanamke akiolewa hazungumzi na mwanamme mwingine kando na mme wake. Aliwekwa kando. Malkia Vashti walikuwa na karamu yao kando.

Siku ya saba ya karamu yake, Mfalme Ahasuero alichangamshwa kwa divai. Mfalme Ahasuero alitaka kuonyesha ukuu wake kwa wakuu na wasimamizi wake. Alikuwa amewaonyesha utajiri na hazina yake yote. Alitaka kuwaonyesha kitu kingine zaidi. Mfalme Ahasuero aliamua kuwaonyesha Malkia Vashti kwa sababu alikuwa wa sura nzuri.



Sitakuja!

Mfalme Ahasuero alituma watumishi wamlete Malkia Vashti kwa karamu yake. Mfalme Ahasuero aliamrisha kwamba Malkia Vashti avae taji ya kifalme ndio aje kwa karamu. Alitaka wakuu na wasimamizi wote waone na watamani uzuri wake. Malkia hakutaka kuenda kwa karamu ya Mfalme. Hakutaka hao watu wote wamwangalie. Malkia Vashti alikataa kwenda.

Mfalme Ahasuero alikasirika sana, Malkia alipokataa kwenda kwa karamu yake. Mtu yeyote hakudhubutu kutotii mfalme. Wakuu wote na wasimamizi walijua kwamba Malkia Vashti alikataa kutii Mfalme. Mfalme Ahasuero alikasirika sana sana. Mfalme Ahasuero aliagiza kwamba Vashti asiwe Malkia tena.

Mfalme Ahasuero alitaka Malkia mpya. Alituma wajumbe kila mahali kwa ufalme wake wote. Wajumbe walileta wanawake warembo kutoka kwa kila eneo la ufalme wake. Mfalme angechagua mmoja wa hao wanawake warembo kuwa Malkia mpya.

Mordekai Myahudi aliishi kwa mji wa Shushani. Mordekai alikuwa mlezi wa binamuye mdogo, Esta. Esta alikuwa yatima. Esta alikuwa mrembo sana. Mordekai alisikia kwamba Mfalme ameamrisha wanawake warembo waende kwa nyumba ya kifalme. Mfalme angechagua mmoja kuwa Malkia mpya. Mordekai aliambia Esta aende na wanawake wengine warembo kwa nyumba ya kifalme. Mordekai aliambia Esta asiambia mtu yeyote kwamba yeye ni Myahudi.

Wanawake warembo wote walikuja kuishi kwa nyumba ya kifalme huko Shushani. Hao wanawake waliongezewa urembo kwa muda wa mwaka moja. Halafu walikuwa tayari kuona mfalme.

Esta aliishi na hao wanawake kwa nyumba ya kifalme. Wanawake hao wengi walikuwa na maringo na hasira. Esta alikuwa mzuri na ana upendo. Esta aliongoja zamu yake aende aone Mfalme.

Esta alienda kuona Mfalme Ahasuero. Mfalme alipenda Esta kuliko wanawake wengine warembo. Mfalme Ahasuero alichagua Esta kuwa Malkia mpya. Mfalme Ahasuero alifanya karamu kubwa. Ilikuwa sherehe ya kuvalisha Esta taji kama Malkia mpya. Alitangaza siku kuu ya mapumziko kwa ufalme wake.

Watumishi wake wawili walikuwa na mpango. Walipanga kua Mfalme Ahasuero. Mordekai alifahamu huo mpango. Mordekai alipelekea Esta huo ujumbe. Aliambia Esta kwamba kuna watumishi wawili waovu wanapanga kua Mfalme. Esta aliambia Mfalme kwamba Mordekai alikuwa amejua huo mpango. Lakini Esta hakuambia Mfalme kwamba Mordekai ni binamu wake.

Wale watumishi wawili waovu walishikwa na kuuawa. Waandishi waliandika habari juu ya wale watumishi waovu na vile Mordekai alikundua mpango wao. Waandishi waliandika kwamba Mordekai alikuwa ameokoa maisha ya Mfalme. Haya yote yaliandikwa kwa vitabu vya kumbukumbu ya Mfalme.

Haya mambo yote yalifanyika kama ya kawaida. Lakini Mungu alikuwa anafanya jambo fulani. Wayahudi ni watu wateule wa Mungu. Mungu huwa anawalinda. Wakati mwingine watu wamejaribu kuangamiza Wayahudi wote. Lakini Mungu huwa anawaokoa. Wakati mwingine Mungu anawaokoa kwa muujiza mkubwa –Mungu aliokoa watu wake kutoka kwa Farao wakati walivuka Bahari ya Shamu kwa nchi kavu. Wakati mwingine Mungu anafanya mambo ili Wayahudi waokoke. Kwa somo lifwatalo tutajifunza vile Hamani aliyejaribu kuangamiza Wayahudi wote. Wakati Esta alikuwa Malkia, hakukuwa na hatari kwa Wayahudi. Kwa somo lifwatalo tutajifunza vile Wayahudi waliokolewa. Tutajifunza vile Esta alisaidia kuwaokoa. Kwa mambo haya yote Mungu alikuwa na mpango wa kusaidia Wayahudi.